

A Dhana ya kuhesabiwa haki.

❖ **What is justification?**

- Paulo anaweka wazi: Mataifa na Wayahudi wote wanahitaji kuhesabiwa haki (maana yake ni, kutangazwa kuwa wenye haki).
- Kuhesabiwa haki kunahusisha nini??
 - (a) Ni kinyume cha hukumu. Mtu aliyehesabiwa haki amesamehewa na kutangazwa kuwa mwenye haki (Kumbukumbu 25:1).
 - (b) Inahusisha kuwa sehemu ya watu wa Mungu.
 - (c) Inahusiana na Mungu na agano lake.

B Njia ya kuhesabiwa haki.

❖ **Matendo ya sheria.**

- Kufanya matendo ya sheria kunadai utimizaji kamili—katika mawazo na matendo pia, katika kila sekunde ya maisha—ya amri zote.
- Hata kama tungefanya hivyo, matendo ya sheria kwamwe yasingetuokoa. Zenyewe ni taratibu tu za maisha na sio njia ya msamaha au ukombozi.

❖ **Kuwa na imani ya Yesu.**

- Imani haihitaji nyongeza ya matendo. Kuhesabiwa haki hakufanyiki kwa Imani na matendo—lkama wafuasi wa dini ya Kiyahudi walivyofundisha—bali nikwa Imani peke yake.
- Imani sio dhana dhahania. Hamna njia yakuwa na Imani tu. Ni lazima uwe na Imani juu ya kitu flani: hiyo ni, kazi Yesu aliyoifanya kwa ajili yetu.
- Imani haijijhesabii haki kwa yenyewe. Imani ni namna tunavyomng'ang'ania Yesu mwenye uwezo wakutufanya tuwe na haki.
- Tumaini letu ni “Imani ya Yesu Kristo.” Tunaokolewa kwa Imani yake na sio kwa imani yetu. Hakuna sifa katika Imani yetu.

C Matokeo ya kuhesabiwa haki.

❖ **Utii wa imani.**

- Imani ya kweli inatoka katika moyo ulioguswa na kusukumwa kumshukuru na kumpenda Mungu kwa wema wake.
- Tunakuwa na Imani baada ya kuipokea na kuikubali kafara kubwa ya Mungu kutupatia uzima wa milele.
- Imani ni muitikio wa upendo wa upendo wa Mungu.
- Kadri Imani inavyokua, sitaki tena kumhuzunisha Mungu kwa kutenda dhambi kwa maksudi.

❖ **Kuendelea kutenda dhambi?**

- Baadhi ya watu walimshutumu Paulo kwa kuisitiza Imani na sio matendo. Walifikiri aliwatia moyo Mataifa kuendelea kutenda dhambi baada ya kuhesabiwa haki.
- Paulo alielewa tu viumbe wapya baada ya kuhesabiwa haki. Sasa Kristo anaishi ndani yetu na tunayatenda matendo Aliyoyaandaa hapo kabla ili tutembea katika hayo(Wagalatia 2:20; 2 Wakorintho 5:17; Waefeso 2:10).